



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA

Tovuti: [www.hlpc.go.tz](http://www.hlpc.go.tz)



## TANGAZO

### KUHUISHA USAJILI (RETENTION) KUPITIA MFUMO WA HPRS

Baraza la Wataalam wa Maabara linachukua nafasi hii kuwakumbusha Wataalam wote wa Maabara wenye usajili wa kudumu kuwa malipo yanafanyika kwa kutumia “**control number**” ambayo ataipata kupitia akaunti yake ya mfumo wa HPRS.

1. Hivyo Wataalam wote mnasisitizwa kufanya malipo ya mwaka kwani malipo haya yanazingatia mwaka wa serikali (1 Julai-30 Juni Mwaka unaofuata).
2. Mtaalam wa Maabara anapaswa kulipia ada ya mwaka Kabla ya tarehe 30 Juni 2023 ili kuepuka adhabu ambapo ni pamoja na mfumo kutamwondoa kwenye kanzi data (Database) hivyo atapoteza usajili wake.
3. Wataalam wote wanatakiwa kufanya malipo ya ada ya mwaka ya kuhuisha usajili (Retention) kama ilivyoainishwa kwenye sheria ya Wataalam wa Maabara Namba 22 ya mwaka 2007 Kifungu cha 32 ikisomwa na kanuni zake za ada na tozo kifungu cha 3(5)
4. Wataalam wa Maabara ambao wana usajili wa kudumu na hawajafunguliwa akaunti watume taarifa zifuatazo kwenye namba **0734005777** ili waweze kuingizwa kwenye mfumo.
  - **Majina Kamili**
  - **Barua pepe (e-mail)**
  - **Namba ya usajili wa kudumu (FRP)**
  - **Namba ya simu**
  - **Ngazi ya elimu ya taaluma.**
  - **Maneno “KUSAJILIWA KWENYE MFUMO KWA AJILI YA KUHUISHA”**

**Angalizo:** Wenye usajili wa awali (PRP) hawahusiki na tangazo hili  
Upatapo tangazo hili mtaarifu na mwenzako.

Imetolewa na ofisi ya Msajili  
Baraza la Wataalam wa Maabara.

